

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MADINI

TUME YA MADINI



TAARIFA KWA WACHIMBAJI NA WAFANYABIASHAYA YA MADINI MKOA WA RUVUMA

Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma inawatangazia wachimbaji na wafanyabiashara ya **MADINI YA DHAHABU NA VITO VYA THAMANI** kuwa soko la madini hayo mkoani Ruvuma litazinduliwa rasmi **tarehe 3 Mei, 2019**. Soko hili limo ndani ya jengo la Ofisi ya Madini Ruvuma lililopo eneo la viwanda karibu na SIDO mjini Singea.

Mara baada ya uzinduzi huo, biashara ya madini husika kwa mkoa wa Ruvuma itakuwa ikifanyika ndani ya soko hili kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa mwaka 2018 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2019. Aidha, hivi karibuni, soko jingine la madini husika litafunguliwa wilayani Tunduru.

Kwa mujibu wa **Kifungu Na. 6** cha Kanuni hizo, mtu yeyote **ATAKAYEBAINIKA KUUZA AU KUNUNUA MADINI NJE YA SOKO LA MADINI** atakuwa ametenda kosa na atastahili kulipa faini ya kiasi cha **MARA TATU YA THAMANI YA MADINI HUSIKA**. Aidha, mkosaji atatakiwa kulipa tozo pamoja na kodi zote stahiki za madini husika kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na **KUTAIFISHWA KWA MADINI HAYO NA KUFUTWA KWA LESENI** ya mkosaji.

Hivyo, wachimbaji na wafanyabiashara wa madini ya dhahabu na vito vya thamani mkoani Ruvuma wanahimizwa kuzingia matakwa haya ya sheria ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

IMETOLEWA NA:

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Jamil'.

KAIMU AFISA MADINI MKOA WA RUVUMA
TAREHE 02 MEI, 2019